

# GRADE 5 END TERM 3 DECEMBER 2021

## KISWAHILI

Jina .....

Jina la shule .....

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

Viwango vya kutathmini				
	Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
Kusikiliza na Kuzungumza	5 <input type="checkbox"/>	4 <input type="checkbox"/>	3 <input type="checkbox"/>	0 - 2 <input type="checkbox"/>
Sarufi	19 - 20 <input type="checkbox"/>	10 - 18 <input type="checkbox"/>	6 - 9 <input type="checkbox"/>	0 - 5 <input type="checkbox"/>
Ufahamu	9 - 10	6 - 8	3 - 5	0 - 2

### I. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (Alama 5)

#### 1. Tunga sentensi ukitumia vitanzandimi vifuatavyo.(alama 2)

- a) Kasa \_\_\_\_\_
- b) Kaza \_\_\_\_\_
- c) Saa \_\_\_\_\_
- d) Zaa \_\_\_\_\_

#### 2. Tegua kitendawili kifuatacho (alama 1)

Bak bandika bak bandua \_\_\_\_\_

#### 3. Kamilisha methali zifuatazo (alama 2)

- a) Mtaka cha mvunguni \_\_\_\_\_
- b) Chanda chema \_\_\_\_\_

## II. UFAHAMU (Alama 10)

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Mlolongo wa magari matano ulikuwa ukipita kwa utaratibu ambapo kando ya barabara, watu waliyatazama magari hayo kwa makini mno kutokana na jinsi yalivyopambwa kwa maua kochokocho.

Miongoni mwa wale waliojipanga barabarani kuyashuhudia hayo, alikuwa kijana Abdala. Ilikuwa ni siku ya Jumamosi alasiri. Gari la kwanza ambalo lilikuwa limepambwa zaidi, liliwabeba bwana na'bi arusi.

- a) Ni magari mangapi yaliyotajwa katika kifungu hiki? \_\_\_\_\_ (alama 1)
- b) Watu walitazama magari wakiwa wapi? \_\_\_\_\_ (alama 1)
- c) Ni nini kilichovutia macho ya watazamaji? \_\_\_\_\_ (alama 1)
- d) Taja mhusika mmoja kati ya walioshuhudia magari hayo \_\_\_\_\_ (alama 1)
- e) Eleza maana ya neno alasiri (alama 1)  
\_\_\_\_\_
- f) Tukio hili lilifanyika siku gani? \_\_\_\_\_ (alama 1)
- g) Gari la kwanza lilibeba akina nani? \_\_\_\_\_ (alama 1)
- h) Eleza aina ya nomino zifuatazo kama zilivyotumika katika kifungu hiki (alama 3)
  - a) Mlolongo wa magari
  - b) Jumamosi
  - c) Gari

**III. SARUFI (Alama 20).**

**Jibu kulingana na maagizo**

**1. Andika wingi wa sentensi hizi. (alama 2)**

a) Mji ulio karibu na kwetu ni huu

\_\_\_\_\_

b) Duka langu lina bidhaa nyingi

\_\_\_\_\_

2. Majira ya baridi kali huitwaje? \_\_\_\_\_ (alama 1)

3. Jibu la lala salama ni \_\_\_\_\_ (alama 1)

**4. Taja mapambo mawili yanayoaliwa kichwani (alama 2)**

i) \_\_\_\_\_

ii) \_\_\_\_\_

5. Tambua nomino za makundi katika sentensi zifuatazo (alama 2)

i) Dobi aliosha tita la nguo chafu \_\_\_\_\_

ii) Genge la wezi lilivamia mzee Busara \_\_\_\_\_

6. Neno 'meza' liko katika ngeli gani? \_\_\_\_\_ (alama 1)

7. Tumia viambishi sahihi (alama 3)

- a) Waraka huo \_\_\_\_\_ likuwa mrefu
- b) Ukurasa wa kitabu \_\_\_\_\_ na picha.
- c) Unywele \_\_\_\_\_ mekatwa.

8. Taja visawe vya maneno yafuatayo. (alama 3)

- a) barabara \_\_\_\_\_
- b) hongo \_\_\_\_\_
- c) mgonjwa \_\_\_\_\_

9. Nyambua vitenzi hivi katika kauli ya kutendewa na kutendeka

(alama 5)

Kitenzi	Kutendewa	Kutendeka
i) Jenga		
ii) Tega		
iii) Imba		
iv) Shika		
v) Ita		